LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
Episode 7: Domestic Violence
Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

Intro:
Ni matumaini yangu kuwa umejiunga nasi katika sehemu nyingine ya mchezo wa kuigiza kwenye makala ya Jifunze Kwa Kusikiliza. Leo Bibiy anapambana na maonevu ya nyumbani dhidi ya wasichana. Karibu kwenye sehemu ya saba ya mchezo kwa jina Ukatili Nyumbani.

CHARACTERS:
Anchor: Intro / Autro
Bibiy..Main Character
Step Mother.....Woman (Adult)
Tamara.......Girl.....14 years
Father.....Male (Adult)
Grandma......same character

Sign Tune.....

SCENE ONE:
(NyumbaniTamara anasikika akiimba huku akifanya kazi za nyumbani)

MOTHER:..Tamara......(Anaitikia kwa mbali (off mic)....Naam mama!)....Tamara....(off mic.....Naam Mama!)
TAMARA: ......Ndio mama naitikia nilikuwa niko huko nyuma .
MOTHER: .... mwangalie msichana huyu mjinga kabisa....unataka nikuite mara ngapi ndio usikie ...Eeh!....Nakuuliza.. nimekuita mara ngapi?.
TAMARA: ...Umeniita mara mbili Mama.
MOTHER:.... (kwa sauti ya kukebehi)....mara mbili Mama....na unafikiria kuwa hiyo ni sawa!...sikiliza kisirani wee hii iwe ndio mara ya mwisho mimi kukuita zaidi ya mara moja..unasikia.
TAMARA: ......Ndio mama!!...

MOTHER: ... Hebu nieleze ulikuwa unafanya nini cha maana huko nyuma ya nyumba?....

TAMARA: .....Nilikuwa namwagilia mimea maji.....kama ulivyoniambia mama kuwa nimwagilie kila baada ya siku mbili.....halafu nilikuwa nikimaliza hapo niwapeleke kondoo mtoni wakanywe maji.

MOTHER: .....Nyamaza, kwanza..nakuuliza mwanangu Jojo amesharudi kutoka shule au bado?

TAMARA: ...hapana bado hajarudi mama..lakini nimewaona watoto wengine wa jirani wamesharudi.

MOTHER: ....Kimya!...funga huo mdomo wako mkubwa kama bakuli la uji....Mimi sikuuliza kuhusu watoto wa majirani...nimekuuliza kuhusu Jojo nduguyo..je?.. umeshamtayarishia kitu chochote cha kula..Mhhh!...

TAMARA: ...Hapana bado.. mama..sijatayarisha chochote lakini nilikuwa nataka kupika uji ili Jojo akitoka shule tu apate kitu cha kunywa..lakini kwanza mpaka nimalize kuchota maji pamoja na kuwapeleka kondoo mtoni.

MOTHER: ......Toka mbele yangu...kimbia haraka ukamalize hizo kazi kisha ujue chakula cha jioni pia kinakungoja kupika..mwangalie msichana mvivu wee..kila kitu mpaka uambiwe.

African Drums........

SCENE TWO:
(Mtoni ndege wanaimba, kondoo wanalia na sauti ya maji yakitirika)

BIBIY: .VipiTamara..hujambo..mambo?

TAMARA: ....Sijambo Bibiy..lakini nimechoka sana

mwenzio..Ooh...mwili wote unaniuma hata sijui nifanyeje, mama yangu wa kambo hata hana huruma na mimi ananifanyisha kazi nyingi kila siku kama punda..ndio maana wakati mwingi nashindwa kwenda shuleni.

BIBIY: ......Tamara ndio maana nimekufuata huku mtoni maanake naona huku ndio mahala pazuri pa mimi na wewe kuzungumza ..Enhee mateso haya umekuwa nayo kwa muda gani sasa?

TAMARA: ..Oh!...Bibiy rafiki yangu hata sijui nikwambie nini..wajua kutoka mama yangu alipofariki na baba akaamua kumleta mama mwingine nyumbani kwetu basi hapo ndipo mashaka yangu yalipoanzia..yaani tangu mama yangu wa kambo aingie nyumbani maisha yangu yamebalika sana.

BIBIY: ..Pole sana Tamara, lakini si unae ndugu wa kiume yule Jojo kwani yeye huwa hakusaidii ...mbona..?

TAMARA: ....(Anamkatiza Bibiy) eti ananisaidia...Hee!!.. Bibiy usitaje hilo jina tena..kwani hujui kuwa Jojo ni mwana mfalme?..mama yangu hataki aguse chochote, anasema kuwa yeye ni mvulana, hivyo basi anahitaji wakati wa kufanya kazi zake za shule...mwenzangu mbona nina shida nyingi mimi.

BIBIY: ...Masikini Tamara... usijali inabidi tutafute njia ya kukusaidia,lakini kwa sasa hebu nikusaidie kuchota maji ili umalize haraka kwani unahitaji kuchota ndoo ngapi zaidi?
TAMARA: .....Ooh! asante sana...ninahitaji kuchota ndoo kumi na mbili zaidi.

MUSIC:

SCENE THREE:
BIBIY: .....Nyanya ninahitaji kumsaidia rafiki yangu.. huyo msichana ana miaka 14 lakini anatumishwa kama mtumwa!

GRANDMA: . ni msichana gani huyo mjukuu wangu hebu nieleze zaidi kumuhusu.

BIBIY: ....Huyo msichana anaitwa Tamara, kwao ni karibu na pale kwenye kichinjio.. ukiwa njiani unaelekea kwenye soko la wanyama umeshapajua nyanya .. sasa huyu msichana huwa haendi shule wakati mwingi kwa sababu anahitajika kufanya kazi zote za nyumbani pamoja na kuwatunza wanyama kila siku.

GRANDMA: ...Mmhh! nimesikia mjukuu wangu lakini nataka ujue kwamba hayo ni maonevu kwa watoto au huo unaitwa ukatili nyumbani dhidi ya watoto....Bibiy, wazazi hawapaswi hata kidogo kuwanyanyasa watoto wao, ni jukumu lao kuwalinda, hata ingawa ni muhimu kwa wazazi kuwafunza watoto wao adabu njema lakini ni muhimu pia kwa wazazi kuona kwamba hawakiuki haki za watoto wao..Ukatili dhidi ya watoto haukubaliki hata chembe.

BIBIY: ....sasa Nyanya tutabadili vipi hali hiyo?..mimi nataka sana kuona kuwa jamii imebadilika.

GRANDMA: ..nashukuru sana kuwa wewe mjukuu wangu ni mtetezi wa haki za wasichana katika mji wetu huu..pia una uzoefu mkubwa kwa kuwa umeshawasaidia wasichana wenzako wengi hadi sasa..kwa hakika unaweza kabisa kumsaidia huyo rafiki yako Tamara.

BIBIY: ...Ni kweli nyanya!!...je naweza kumuuliza mwalimu kama tunaweza kuandaa maonyesho au mchezo wa kuigiza ili kuangazia maonevu dhidi ya watoto hasa wasichana?

GRANDMA: ..mjukuu wangu hilo ni wazo zuri sana..ukatili dhidi ya watoto ni jinamizi linalo poteza maisha ya watoto na ni adui wa familia.

BIBIY: ..lakini nyanya kwa nini kina mama wengine wanawatesa watoto wao?.

GRANDMA: .....Ni kwa sababu baadhi ya kina mama ndio wakiukaji wakubwa wa haki za watoto wao hasa watoto wa kike..wanawanyima haki ya kupata elimu, wengine wanawanyima chakula na pia kuwafanyisha wasichana kazi nyingi kupita kiasi..Bibiy, kwanza ni lazima umweleze mwalimu kuhusu matatizo ya rafiki yako Tamara ili achukue hatua zinazostahili umesikia mjukuu wangu.

BIBIY: ...Ndio nyanya, asante sana kwa ushauri wako..sasa naomba ruhusa niondoke kwani nina miadi na rafiki zangu, tunakwenda kumsaidia Tamara.

GRANDMA..sawa Bibiy usichelewe sana leo napika chakula kitamu.

MUSIC.....

SCENE FOUR:

FATHER: .Tamara mwanangu ..mwalimu wako ameniita kunilalamikia kuwa wewe siku hizi umekuwa mtoro na hufiki shuleni mara nyingi je unaweza kunieleza kwa nini unakosa kwenda shule mara kwa mara siku hizi?

TAMARA: .....Baba ni kweli kuwa mimi siku hizi mara nyingi huwa siendi shule, lakini ni kwa sababu mama huwa ananipa kazi nyingi hapa nyumbani kila siku.. kazi za shambani zinaningoja mimi na pia kuwapeleka wanyama mtoni kila siku.. sasa ni saa ngapi nitaenda shule mimi?

FATHER: .Tamara..una hakika hayo unayoniambia ni ya kweli!!....ni kwa muda gani yote haya yamekuwa yakiendelea? Eeh!

TAMARA: ....Kila siku baba tangu nilipompata mama huyu mpya!.

FATHER: ....Ni sawa nimekusikia mwanangu.sasa nataka

upeleke barua hii kwa shangazi yako halafu ukirudi baadaye tutazungumza zaidi.

TAMARA: ...Sawa baba wacha niende , nitarudi haraka. (Mlango unafungwa).

FATHER:.Mama Tamara..mama Tamara!!....Uko wapi.

MOTHER:....Abee niko hapa, unasemaje mume wangu.

FATHER: ......Hebu tafadhali kaa hapa ninataka kuzungumza na wewe..mke wangu nilikuwa shuleni kwa kina Tamara leo..mwalimu analalamika kuwa binti yetu hafiki shuleni siku hizi..mimi siko hapa kwa muda mrefu kwa sababu za kikazi..hebu nieleze inakuwaje Tamara anakosa kwenda shuleni na mwenzake Jojo anakwenda kila siku?

MOTHER: ......Ndio kwa sababu hao watoto wawili sio sawa...Jojo ana bidii sana ya masomo lakini Tamara.....Hee!! ni mvivu sijapa kuona..nafikiri hapendi shule.

FATHER:....Lakini mke wangu mbona nikiwa hapa Tamara anakwenda shule kila siku?

MOTHER..ni wazi kuwa anakuogopa!!.....

FATHER:....Mke wangu unaniambia kweli au unanidanganya..au labda Tamara haendi shule kwa kuwa ana majukumu mengi hapa nyumbani?..nasikitika kuwa nimemuhoji mototo nae amenieleza kila kitu..mke wangu kwa nini unamtesa mototo wetu bila sababu, wako wapi wafanyakazi tuliokubaliana kuwa utawa ajiri?

(Mlango unagongwa)........

MOTHER: ...karibu pita ndani.

FATHER: ...Ooh Bibiy pamoja na wenzako karibuni piteni ndani.

BIBIY: ....Asante, shikamoo...tumekuja kumtembelea Tamara..yuko?

FATHER:..hapana hayuko lakini atarudi sasa hivi.

BIBIY: ....Au amekwenda kuchota maji? Maanake tulikuwa tumekuja kumsaidia..juzi nilimsaidia kuchota ndoo kumi na mbili.

FATHER: ..Alaa kumbe!!....Mama Tamara unasikia hayo?

MOTHER: ..Eti nimesikia nini?

BIBIY: ..nasema juzi nilimsaidia Tamara kuchota maji ndoo kadhaa na kila siku sisi huja kumsadia kuchota maji na kufanya kazi zingine, mwalimu pia anatuuliza kwa nini Tamara haji shuleni, mimi nilimuuliza siku moja nae akaniambia kuwa mama yake huwa anampa kazi nyingi za kufanya lakini kaka yake Jojo anakwenda shule kila siku hajui ni kwa nini yeye anabakia nyumbani.

MOTHER: ....haya basi uliyoropoka yametosha tokeni mwende zenu manaake huyo rafiki yenu Tamara hatarudi sasa..na wewe mwenye nywele kama kamba anza kuongoza msafara.

FATHER: .....Mama Tamara watoto hawa hawatakwenda popote mpaka rafiki yao atakaporudi ili tulitatue tatizo hili. (Mlango unafunguka-Tamara anaingia).

TAMARA: ....Hi!!...rafiki zangu nimefurahi sana kuwaona karibuni..baba unasalimiwa na shangazi.

BIBIY: ..Tamara tulikuwa tunakungojea wewe, tumekuja kukusaidia kazi zako.

FATHER: Bibiy hakuna kazi yoyot leo nendeni nje mkacheze. (Mlango unafungwa)

FATHER: ....Enhee...Mama Tamara sasa nataka unieleze

mambo haya yameendelea kwa muda gani?...je unafahamu kuwa umemtendea mototo wetu unyama wa hali ya juu..unajua kuwa hayo ni maonevu..mke wangu mimi nimekuoa kwa sababu nakupenda na pia nilijua Tamara binti yangu amepata mama kama vile mimi ulivyokabidhi mwanao Jojo.. kwa nini unawabagua watoto?

MOTHER: ....Basi mume wangu yaishe naomba samahani..nimetambua kuwa nilikuwa namtesa Tamara bure tu, sikumtendea haki hata kidogo.ni kweli kuwa nilimtumisha kupita kiasi hadi akawa anashindwa kwenda shuleni...samahani sana mume wangu nimekosa.

FATHER: ....ujue kuwa watoto ni baraka na ni jukumu letu wazazi kuwapenda na kuwalinda watoto..isitoshe watoto wa kike ni sawa tu na watoto wa kiume wana haki ya kupata elimu sawa ilikuwa huna haja ya kumtesa Tamaa masikini tena amefiwa na mama yake juzi juzi tu kwa nini humuonei huruma.

MOTHER: ..Ooh!!...mume wangu basi usiseme yote hayo mimi najilaumu sana nimekosa na ninakuahidi sitarudia tena. Tokea leo Tamara na Jojo watakuwa sawa machoni mwangu.
African Drums......

(wasichana wanazungumza nje)

BIBIY: ..Nyanya yangu alinihadithia kuwa utotoni mwake wazazi waliwageuza kuwa ni wasaidizi wa nyumbani tu lakini amesema anashangaa sana kuona kuwa katika ulimwengu ulio endelea bado kuna wazazi wanaowatesa binti zao.

TAMARA: . Bibiy baba yangu aliniuliza nami nikamwambia kila kitu sikumficha.

BIBIY: ..Alaa!..Kwa hiyo kabla hujatoka ulikuwa tayari umesha mwelezea baba yako kila kitu..hee mambo yalijipanga nakwambia.. namimi nyanya yangu alikuwa ameniambia nije

kwenu halafu kwa vyovyote vile nimwage mtama ili baba yako ajue kuwa unateseka.

TAMARA: ...Na kwa vile leo sijaambiwa kufanya kazi zozote nadhani mpango wetu umefaulu.

BIBIY: ....Nina hakika tumelitatua tatizo hili.loo rafiki yangu utakuwa ni msichana mwenye furaha tena! Lakini kumbuka Tamara yote haya yamewezekana kwa kuwa ulikuwa huna uoga wa kuzungumza ukweli wewe unajiamini..waeleze wasichana wengine kila mara kuwa lazima tujiamini hii inasaidia sana. .kila mara tunapokuwa na matatizo lazima tuzungumze na mtu sio tu kujinyamazia.

TAMARA.: ....Bibiy...hata sijui nikushukuru vipi rafiki yangu.yaani nimefurahi sana kuwa nafikiri sasa nitaweza kurudi tena shuleni...nauliza kama naweza kujiunga na kikundi chenu cha Gir Power?

BIBIY: ...Ndio unaweza Tamara. Mikono yetu iko wazi kukupokea..kesho tunakwenda kwenye internet cafe kwa hivyo unakaribishwa tunaweza kwenda pamoja ukipenda.

TAMARA: ...Je huwa mnafanya nini huko kwenye internet cafe?

BIBIY: ....Tunatafiti mambo mengi..unajua Tamara kwenye mtandao unaweza ukapata taarifa nyingi tu na pia kujua ni yapi yanayo endelea ulimwenguni, naam itabidi tukuache sasa.. bye...bye Tamara!! Tutaonana kesho.

END

Autro: Naam msichana Tamara ameokolewa kutoka kwenye minyororo ya mateso na hatimae atarudi tena shule kuendelea na masomo. Je wewe umejifunza nini? Sina shaka utaungana nasi tena wiki ijayo katika makala haya ya Jifunze Kwa Kusikiliza. Sikiliza tena mchezo huu au mdokeze rafiki yako nae

ausikilize katika tovuti yetu kupitia anuani ifuatayo www.dw-world.de/lbe .. Hadi wiki ijayo kwaheri.